Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# JARIDA

**LA MTANDAONI** | TOLEO LA JUNI 2023

## SEMINA KWA WAHESHIMIWA MAJAJI NA MAHAKIMU

KANDA YA ZIWA, TABORA, MANYARA NA KIGOMA




Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

**NSSF**

Simu Bure 0800116773

@NssfTanzania




## NSSF YAENDESHA SEMINA KWA WAHESHIMIWA MAJAJI NA MAHAKIMU JIJINI MWANZA

## **Jaji Kiongozi:** "NSSF imefungua njia wadau wengine wafuate"

**Na MWANDISHI WETU**

Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mhe. Mustapher Siyani amewataka Waheshimiwa Majaji na Mahakimu nchini kuyapa kipaumbele mashauri yote yanayohusu sekta ya hifadhi ya jamii.

Mhe. Jaji Kiongozi Siyani alisema hayo Juni 9, 2023 wakati akifungua semina ya siku mbili kwa njia ya ***e-Mikutano*** kwa Waheshimiwa Majaji na Mahakimu wa Kanda ya Ziwa, Tabora, Manyara na Kigoma iliyofanyika jijini Mwanza.

Alisema kupitia semina hiyo NSSF imefungua njia ambayo wadau wengi wataifuata, hivyo Mahakama na NSSF kama ilivyo kwa taasisi nyingine zinazotoa huduma kwa jamii haziwezi kufanikiwa ikiwa kila taasisi itajifungia ikiamini inaweza.

"Niwahakikishie wadau wetu wote wakiwemo NSSF kuwa Mahakama ya Tanzania itaendelea kuwashirikisha katika mipango yake na hususan inapotekeleza mpango mkakati wake wa miaka mitano utakaokamilika ifikapo mwaka 2025," alisema.



**Inaendelea ...**

Mhe. Jaji Kiongozi Siyani alisema kupitia kikao hicho Waheshimiwa Majaji na Mahakimu watapata fursa nzuri ya kujadiliana na kubaini mambo mbalimbali ambayo yatasaidia kurahisisha na kuongeza kasi ya usikilizwaji wa mashauri katika maeneo mbalimbali hasa yanayohusu sekta ya hifadhi ya jamii.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani, Godfrey Ngonyani, alisema ushirikiano baina ya Mfuko na mhimili huo ni muhimu na ni sehemu ya mkakati wa NSSF kuendelea kushirikiana na wadau, ikiwemo kuandaa vikao na semina.

Ngonyani alisema Mfuko umekuwa ukishirikiana na Mahakama kupitia ziara ambazo zilifanywa Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini na zinatarajiwa kuendelea katika kanda nyingine na kwamba Mahakama ni wadau muhimu kwenye mashauri dhidi ya waajiri wanaokiuka sheria kwa kushindwa kuwasilisha michango kwa wakati.

# UCHELEWESHAJI WA MICHANGO KATIKA MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII UNAZOROTESHA HAKI

**Na MWANDISHI WETU**

Chama Cha Majaji na Mahakimu Tanzania (JMAT), kimesema ucheleweshaji wa michango ya wanachama unaofanywa na baadhi ya waajiri katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii unazorotesha haki za wanaostahili kupata mafao yao kwa wakati.

Hayo yamesemwa na rais wa JMAT, Mhe. Jaji John Kahyoza ambaye pia ni Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Manyara wakati wa semina ya siku mbili iliyofanyika tarehe 9 hadi 10 Juni 2023 jijini Mwanza. Semina hiyo iliandaliwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kwa ajili ya majadiliano ya pamoja baina ya Mfuko na Waheshimiwa Majaji pamoja na Mahakimu wa Kanda ya Ziwa, Tabora, Manyara na Kigoma iliyokuwa na kauli mbiu isemayo **"UTOAJI HAKI KWA WAKATI KWA USTAWI WA HIFADHI YA JAMII"**.

"Kupitia semina hii tumejifunza kuwa ucheleweshaji wa michango katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii unazorotesha uchumi na haki za wanaostahiki kupata mafao," alisema Mhe. Jaji Kahyoza.

Alisema katika semina hiyo waligusia maeneo mbalimbali juu ya uendeshaji wa Mifuko, changamoto inazokabiliana nazo, namna nzuri ya kuzitatua, pia wanachama wa JMAT wameweza kufahamu mafao yanayotolewa na NSSF pamoja na mchango wa Mahakama katika kuhakikisha ustawi wa hifadhi ya jamii unazidi kuimarika.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Sheria wa NSSF, Geoffrey Sikira alisema Mfuko unayo mashauri 350 katika mahakama mbalimbali yakiwemo yanayohusiana na madai ya michango yaliyoshindwa kuwasilishwa na waajiri na hivyo kusababisha wanachama kushindwa kupata haki zao kwa wakati.



Mhe. Jaji John Kahyoza, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Manyara ambaye pia ni rais wa JMAT, akizungumza wakati wa semina hiyo

# HABARI KATIKA PICHA




Mgeni rasmi Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mheshimiwa Mustapher Mohamed Siyani (akiwa katika picha ya Mkutano mtandaoni) akifungua semina ya siku mbili kwa Waheshimiwa Majaji na Mahakimu wa Kanda ya Ziwa, Tabora, Manyara na Kigoma kwa njia ya mtandao kupitia ***e-Mikutano*** kwa lengo la majadiliano kuhusu sheria na majukumu ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye
Simu Bure
0800116773

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye
SMS
15200

Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye
NSSF Taarifa Whatsapp
+255 756 140 140

# MATUKIO KATIKA PICHA













Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# TAARIFA KWA UMMA

## KUANZISHWA KWA OFISI MPYA YA NSSF UBUNGO NA KUHAMA KWA OFISI YA NSSF KINONDONI

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), unapenda kuwataarifu Wanachama, Waajiri na Umma kwa ujumla kuhusu kuanzishwa kwa Ofisi mpya ya NSSF Ubungo katika jengo la Ubungo Plaza. Ofisi hii imeanza rasmi kutoa huduma tarehe 1 Juni, 2023.

Aidha, Ofisi ya NSSF Kinondoni iliyokuwa kwenye jengo la Ubungo Plaza imehamishiwa kwenye jengo la Millenium Tower lililopo eneo la Makumbusho - Kijitonyama. Ofisi hii imeanza rasmi kutoa huduma tarehe 1 Juni, 2023.

Lengo la kuanzishwa kwa ofisi mpya ya Ubungo na kuhamishwa kwa ofisi ya Kinondoni ni kusogeza huduma zitolewazo na Mfuko karibu zaidi na wateja.

Kwa maelekezo zaidi wasiliana nasi kupitia simu ya bure 0800116773 au tembelea ofisi ya NSSF iliyo karibu nawe.

**Imetolewa na:**

**Kitengo cha Uhusiano na Elimu kwa Umma**

BOARD OF TRUSTEES
NSSF
NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND

**Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye**

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

# NSSF